Nia Dhidi Yetu Wenyewe Sehemu Ya 1 “Kujichunguza Wenyewe”

na

Ellis P. Forsman

Nia Dhidi Yetu Wenyewe Sehemu Ya 1 “Kujichunguza Wenyewe”

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 6, 2011

Nia Dhidi Yetu Wenyewe Sehemu Ya 1 “Kujichunguza Wenyewe”

2 Kor. 13:5

Nia njema kimsingi ni muhimu. Ni muhimu kwa ajili ya umoja katika kusanyiko la sehemu moja.

Tulijifunza nia yetu dhidi ya Mungu, Yesu Kristo, Injili, Kanisa, na Ndugu zetu; sasa tutajifunza nia dhidi yetu wenyewe (somo lililo na sehemu 2).

Ebu tuangalie baadhi ya nia tunazotakiwa kuwa nazo miongoni mwetu sisi wenyewe.

Kama Yeremia alivyoulilia mji wa Yerusalemu ulipokuwa unaangamizwa, aliwaita watu wajichunguze wenyewe na wamrudie Bwana.

Ombo. 3:40-41, “*Na tuchunguze njia zetu na kuzijaribu, na kumrudia BWANA tena. Na tumwinulie Mungu aliye mbinguni mioyo yetu na mikono.*”

Katika kufundisha juu ya kushiriki katika meza ya Bwana, Paulo aliandika kwamba ulikuwa ni wakati wa mtu kujichunguza mwenyewe.

1 Kor. 11:27-30, “*Basi kila aulaye mkate huo na kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana. Lakini mtu ajihoji mwenyewe na hivyo aule mkate na kukinywea kikombe. Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake kwa kutokuupambanua ule mwili. Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, na watu kadha wa kadha wamelala.*”

Baadaye Paulo aliwatia changamoto Wakorintho wajichunguze wenyewe.

2 Kor. 13:5, “*Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu? Isipokuwa mmekataliwa.*”

Katika kufanya hivyo, anatumia wakati uliopo katika neno “*jichunguze*” na “*thibitisha*”, ikionyesha kwamba kujichunguza huko lilikuwa endelevu!

Kiasili swala hili linaweza kuibua maswali muhimu…

Kwa nini tunapaswa kujichunguza wenyewe? Kwa kiwango gani tunapaswa kujichunguza wenyewe? Ni maswali ya aina gani tunayopaswa kujiuliza wenyewe?

Katika somo hili, ningependa tuangalie umakini wetu katika wito huu wa "Kujichunguza Mwenyewe". Tunapofanya hivyo, hebu tujibu maswali ambayo tayari yameibuliwa, tukianza na…

Kwa nini tunapaswa kujichunguza wenyewe?

Kujua kama tupo katika imani

Paulo alisema katika 2 Kor. 13:5, "*Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu? Isipokuwa mmekataliwa.*"

Neno "*katika imani*" inamanisha kuwa Mkristo mwaminifu.

Hivyo tunapaswa kujichunguza kama tuko au hatuko katika imani ndani ya Bwana! Tunapaswa kukumbuka kwamba hatari ya kuacha kanisa mara zote ipo. Ni rahisi kuacha kama tukiukana wokovu wetu.

Ebr. 2:1-4, "*Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa tusije tukayakosa. Kwa maana ikiwa lile neno lililonenwa na malaika lilikuwa imara, na kila kosa na uasi ulipata ujira wa haki, sisi je! Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitishwa kwetu na wale waliosikia; Mungu naye akishuhudu pamoja nao kwa ishara na ajabu na nguvu za namna nyingi, na magawanyo ya Roho Mtakatifu, kama alivyopenda mwenyewe.*"

Wahubiri wa ulimwengu wa dini udharau injili ya Kristo na badala yake wanaleta hadithi za wakati wa kulala, nyimbo za shule za awali, hotuba ndogo, na kuingiza saikolojia, filosofia, matukio, na siasa. Mambo haya hayawezi kuushawishi ulimwengu wa dhambi; na haziwezi kuongoa mioyo kwa Kristo.

Viongozi wengi wa dini ulimwenguni leo hawayakubali mamlaka ya maandiko kuhusu mpango wa Mungu wa wokovu. Hata mhubiri mmoja wa kanisa la Kristo katika jarida moja la kanisa nililopokea alijisifu kwamba alihubiri kwa mwaka mzima bila kutaja ubatizo mara moja. Hii haifanani na injili ya kwanza iliyohubiriwa na Petro ambapo ubatizo ulifundishwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi.

Wengi sana wanaridhika wanaporuhusu jamii ivutie injili yao kuliko kuruhusu injili ya Kristo ivutie jamii yao. Hata makanisa ya Kristo yamebadilika kwa miaka. Kulikuwa na wakati ambao makanisa yote ya Kristo yalikutana kama tunavyofanya. Alafu yakaanguka katika mvuto wa dini za kikanisa za ulimwengu na wakarekebisha vitu vingi katika ibada ambazo hayajaruhusiwa katika maandiko.

Huko nyuma katika mwaka wa 1925, Ndg. George Scott, babu yake na kaka yangu, akwenda Kaskaini mwa Rhodesia katika Afrika na akatengeneza misheni. Yeye, kwa msaada wa wengine, walitafriri Biblia kwa lugha ya wenyeji. Walitumia kikombe kimoja tu katika ushirika wa meza ya Bwana. Baada ya miaka 20 akarudi Marekani kusalimia, na aluhuzunishwa sana kwa kiwango ambacho kanisa lili badilika kwa wakati mfupi baadaye akarudi Afrika akakaa hadi alipofariki mwaka wa 1955. makanisa mengi ya Kristo ulimwenguni kote leo wameachana na injili tangia hapo.

Sababu moja inayosababisha vijana wengi leo wanaacha kanisa ni kwamba wanataka kuburudishwa, badala ya kumwabudu Mungu.

Ninapaswa kuhusisha ujuzi niliopokea nilipokuwa nikiudhuria ibada ya jioni katika kanisa fulani jirani yetu ambapo mke wangu, Lynell na mimi tulialikwa. Ibada ilipoanza watoto wote walio na umri tofauti waliongozwa kwenda katika madarasa yao ambapo mochoro nyingi ilikuwa ikiwasubiri. Watu wazima walibaki katika jengo la ibada na "walihudumiwa" katika kiwango cha kuunda bendi ya muziki, kijana mwimbaji, na msaidizi mwanamke. Hakuna vitabu vya nyimbo vilivyokuwepo kwa ajili ya "walioudhuria" kushiriki. Muziki huo ulikuwa na "hisia" na mapigo, lakini ikiwa na ubora kidogo wa kimaandiko.

Mhubiri alitembea miongoni mwa wale waliokuwa mbele alipokuwa akinena, akiwagusa na kuwapiga piga begani mwao, labda ili kuwafanya wajisikie "imara." Aliongea kwa kutia moyo walioudhuria ili waishi maisha makuu, akitoa mifano ambayo haipo kibiblia. Alitumia mistari miwili tu katika Biblia ndani ya mazungumzo yake na vyote akazielezea tofauti.

Mistari aliyotoa ni pamoja na Eze. 1:4-6, "*Nikaona na tazama upepo wa dhoruba ulitoka upande wa Kaskazini, wingu kubwa sana pamoja na moto ukifanya duara ya nuru na mwangaza pande zote, na katikati yake kitu kama rangi ya kaharabu, katikati ya moto huo. Kukatokea katikati yake mfano wa viumbe hai vinne, kuonekana kwao kulikuwa hivi; walikuwa na sura ya mwanadamu. Na kila mmoja alikuwa na nyuso nne, na kila mmoja alikuwa na mabawa manne.*" Soma kitabu cha Ezekieli na utaona kwamba kuna maelezo mengi zaidi kuhusiana na wanyama kuliko maelezo haya ya mhubiri huyo.

Kwa burudani ya nyongeza katika ibada yote, mchoraji pale mbele alijaribu kunasa mawazo ya watu kwa kupaka rangi picha kubwa ya mnyama kulingana na andiko lililosomwa na mhubiri. Ikatokea tofauti na maelezo yaliyotolewa na Ezekieli hazikufanana. Mchoraji huyo pia akaweka picha ndogo ya mtu chini kwenye kona ya mchoro, akionyesha kwamba Ezekieli anamtazama mnyama.

Mhubiri huyu alidai kwamba Ezekieli hakujua ni mnyama wa aina gani, na kwamba kilikuwa ni kitu kikubwa ambacho kilistahili kuabudiwa, hivyo Ezekieli alianguka chini na kukiabudu. Nikafikiria mwenyewe, “Kitu hakiko sawa na picha hii.”

Kwa haraka nikaweka fikra zangu katika kitabu cha Ezekieli na siku shangazwa kupata kwamba Ezekieli hakuabudu mnyama. Kwa hakika, sura ya 10 ya Ezekieli inasema mnyama ambaye Ezekieli alimwona katika maono ilikuwa ni makerubi manne. Unafikiri kwamba kama Ezekieli angeabudu mnyama huyu, Mungu alisema kwamba anawivu na akaagiza kwamba ni yeye pekee ndiye anapaswa kuabudiwa.

Mhubiri huyu alijaribu kufanya ibada ivutie, lakini haikuwa na mwongozo mzuri.

Lynell akaniambia kwamba alikuwa hajisikii kuwepo pale. Nami nikamwambia siyo tu kujisikia vizuri kuwa pale, bali pia nilichukia kwa sababu mhubiri huyu alikuwa anawadanganya watu hawa. Vifungu viwili tu katika hotu yote, na walidanganywa! Ni huzuni kwamba hili ndiyo swala iliyopo katika ulimwengu wote wa kidhehebu. Je! Wahubiri kama hawa wanaionea haya injili ya Mungu wanapoificha katika mahubiri yao?

Paulo alisema katika Rum.1:16, “*Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Munu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia.*” Pia akasema katika 2 Kor. 4:3, “*Lakini ikiwa Injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wanaopotea;*” imesitirika kwa sababu imekosekana katika hotuba zao.

Je dhamira za wahubiri hawa huchomwa, kwa sababu hawaonekani kujali kile wanachokifanya au kusema kadiri wanavyopata majibu ya matakwa yao? Je nia hii ya “mwisho kusafisha njia” umpendeza Mungu?

Nilipokuwa kijana mdogo katika kanisa, nilitembelea mkutano wa Injili wa Kibaptist pamoja na Ndg. Howard McCay. Wakati wa hotuba mhubiri alifundisha dhana kwa ukweli kwamba Biblia iliponyamaza. Alipotoa mwaliko mwishoni mwa hotuba yake akawaambia kila mmoja kufumba macho na ye yote ambaye angependa amwombe Mungu kwa niaba yao wafanye ijulikane kwa kunyoosha mikono yao. Sikufumba macho vizuri na nikainamisha kichwa chini, alafu nikasikia mhubiri akisema, “Mungu akubariki, ndugu!” “Mungu akusamehe, dada!” au kitu kinacho fanana na hicho, alafu akahitimisha kwa kusema, “Sasa kumbukeni, nataka kila mmoja aheshimu usiri wa wengine na wafumbe macho.” Baada ya hapo Ndg. Howard akaniambia kwamba alikuwa akimwangalia mhubiri akitangaza baraka zake kwa watu ambao hawakunyoosha mikono yao, hivyo akaangalia katika macho ya muhubiri kinaganaga. Uongo wa mhubiri huyu ulijulikana, na bado

anaendeleza uongo huo. Ibada ilipokwisha alimkwepa Ndg. Howard. Uongo kama huo ni maarufu miongoni mwa ulimwengu wa kidhehebu.

Kwa nini watu wengi wanapenda dini zinazodanganya? Ni kwa sababu wanahitaji dhamira isiyo sumbuliwa; hivyo hawachunguzi wanachofundishwa. Iwe wanaijua au hapana, kwa kiburi hawamtii Mungu na Injili yake, na mara watapotea kama wasipobadilika.

- 2 Thes. 1:7-8, "*Na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi, wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu.*"

- 2 Thes. 2:10, "*Na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa.*"

Ni aibu kwamba wengi wangependa kusikiliza ujumbe ulio rahisi, ujumbe ambao hauhukumu badala ya kusikiliza neno la Mungu. Paulo alimwambia Timotheo (na kwetu sisi pia) kuhubiri neno la Mungu, na siyo ujumbe mwingine ambao ungesikika vyema masikioni mwao. "*Nakuagiza mbele za Mungu na mbele Kristo Yesu atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake; lihubiri neno uwe tayari wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho. Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli na kuzigeukia hadithi za uongo.*" (2 Tim. 4:1-4).

Kuwa macho! Kama muhubiri ye yote wa dhehebu akihubiri swala lingine na kuacha neno la Mungu, ni mbwa mwitu aliyevaa mavazi ya kondoo. Haijalishi hata kama inasikika vyema, au inawachangamsha watu, mtu huyo ni wakili wa uongo wa neno la Mungu.

Kama ye yote akiwa na nia kwamba hawaridhiki na kanisa la Kristo, unapaswa kuchunguza kwa karibu ni nini chaguo lako. Kanisa lolote linapaswa kufanana na maelezo ya bibi arusi wa Kristo tuliyojadili siku chache zilizopita, la sivyo siyo bibi harusi wa Kristo.

Inawezekana kujenga moyo mbovu wa kutokuamini. Ebr. 3:12-14, "*Angalieni, usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai. Lakini mwonyane kila siku, maadamu iitwapo leo; ili mmoja wenu asifanywe mgumu kwa udanganyifu wa dhambi. Kwa maana tumekuwa washirika wa Kristo, kama tukishikama na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho;*"

Kile ambacho andiko hili humaanisha, hataivyo, ni kwamba inawezekana KUFAHAMU msimamo wa mtu mbele za Mungu. Hakika, Biblia iliandikwa kwa kusudi hili, ili kwamba tufahamu.

Kitabu kimoja binafsi ina kusudi hili katika wazo. 1 Yoh. 5:13, "*Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu.*"

Hiki ni kitabu chenye jaribio lililo wazi. Tumepewa majibu. 1 Yoh. 3:24, "*Naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye naye ndani yake. Na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa huyo Roho aliyetupa.*"

Kujua kama Yesu Kristo yu ndani yetu.

Paulo aliwatia changa moto Wakorintho kuzingatia kama Yesu Kristo alikuwa ndani yao. Hilo ni wazo la ajabu tunapofikiria kwamba Kristo anakaa ndani ya Wakristo.

Iliahidiwa na Yesu mwenyewe Yoh. 14:21-23, "*Yeye aliye na amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake. Yuda (asiye Iskariote) akamwambia Bwana imekuwaje ya kwamba wataka kujidhihirisha kwetu, wala si kwa ulimwengu? Yesu akajibu akamwambia mtu akinipenda atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake na kufanya makao kwake.*"

Inaanza pale tunapomvaa Kristo katika ubatizo. Gal. 3:26-27, "*Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*"

Tunaweza kushangaa kwa nyakati "jinsi" anavyokaa ndani yetu lakini swala la msingi hapa ni kufahamu kwamba anakaa! Kutambua kwamba kuna njia tunazoweza KUFAHAMU kama anakaa! Ndiyo maana tunahitaji kila mara tujichunguze wenyewe!

Kwa nini tunapaswa kujichunguza wenyewe? Ili kujua kama "*tumekataliwa*" (hatuna sifa). 2 Kor. 13:5, "*Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu? Isipokuwa mmekataliwa.*"

Imetolewa kwamba Kristo yu ndani ya Wakristo, isipokuwa "*wamekataliwa*".

"*Kukataliwa*" kuna maanisha nini? Yafuatayo ndivyo tafsiri zingine husema…

- "*mmekataliwa*" (KJV).
- "*umeshindwa jaribio* (NIV). (Kumbuka nilisema kwamba ni kitabu chenye mtihani wa wazi. Tunaweza kujua kama tumefaulu au tumeshindwa)
- "*isipokuwa hakika kama mmeachwa*" (NKJV).

Kialisi, "*huwezi jaribio*", na katika mazingira inazungumzia jaribio la…

- Kuwepo katika imani.
- Kuwa na Kristo ndani yako.

Kifungu hiki ni moja kati ya ile inayofunua kwamba Mkristo anaweza kuanguka mbali kutoka katika neema!

Paulo alionya kuhusu kuanguka kutoka katika neema. Gal.5:4, "*Mmetengwa na Kristo ninyi mtakao kuhesabiwa haki kwa sheria* (Sheria ya Musa); *mmeanguka na kutoka katika hali ya neema.*"

Yesu alielezea kile ambacho kingetokea kwa yale matawi ambayo hayakuzaa matunda. Yoh.15:6, "*Mtu asipokaa ndani yangu hutupwa nje kama tawi na kunyauka watu hutakusanya na kuyatupa motoni yakateketea.*"

Tena, kupitia mtu kujihoji mwenyewe anaweza KUFAHAMU sharti la kweli ni nini!

Kwa nini tujihoji wenyewe? Ili kujua kama tunajifahamu wenyewe. Kama Paulo anavyotowa wito wa mtu kujichunguza mwenyewe, anauliza "*Hamjijui ninyi wenyewe?*"

Tunaweza kuanguka katika mtego wa kujidanganya kirahisi. Yako. 1:22-25, "*Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu. Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo. Maana hujiangalia kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo. Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.*"

Dini ya mtu kama huyo ni "*bure*" (haifai). Yako. 1:26, "*Mtu akidhani ya kuwa anayo dini, wala hauzuii ulimi wake kwa hatamu, hali akijidanganya moyo wake, dini yake mtu huyo haifai.*"

Isipokuwa kila mara mtu ajihoji kunaweza kuepusha <u>kujidanganya wenyewe</u>!

Kwa hiyo hitaji mara zote ipo katika "*kujichunguza mwenyewe*", katika "*kujithibitisha wenyewe*". Hiyo utuongoza katika swali lifuatalo…

Ni kwa kiwango gani tunapaswa kujihoji wenyewe?

Kimsingi, siyo kwa kujikadiria wenyewe. Hatuwezi kuamini katika kile ambacho tunafikiria wenyewe. Tunathibitishwa tu ikiwa Bwana ametukubali. 2 Kor. 10:18, "*Maana mtu mwenye kukubaliwa si yeye ajisifuye, bali yeye asifiwaye na Bwana.*"

Hivyo hata kama tunaweza "kufikiria" kwamba tuko sawa, sisi siyo kipimo cha mwisho.

Paulo aliandika katika 1 Kor. 4:4, "*Maana sijui sababu ya kushitaki nafsi yangu, lakini si hesabiwi haki kwa sababu hiyo; ila anihukumuye mimi ni Bwana.*"

Tunaweza kukosea katika fikra zetu, na ikatuongoza katika hitimisho isiyo sahihi dhidi yetu wenyewe.

Wakati fulani Paulo alifikiri kwamba kuwatesa Wakristo kulimpendeza Mungu, lakini Yesu alimwambia kwamba hakuwa sahihi tunaposoma katika Mdo. 26.

Kutakuwa na watu wengi katika hukumu waliofikiri kwamba walimpendeza Mungu wakati wa maisha yao.

Mat. 7:21-23, "*Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu.*"

Hivyo lazima tuangalie kiwango nje yetu sisi wenyewe ambayo ndiyo tutajichunguza wenyewe! Hatupaswi kutumia makadirio ya watu wengine. Hatuwezi kujilinganisha na wengine, au kuamini uthibitisho wao.

Kujilinganisha na wengine siyo busara. 2 Kor. 10:12, "*Kwa kuwa hatuthubutu kujihesabu pamoja na baadhi yao wanaojisifu wenyewe, wala kujilinganisha nao; bali wao wenyewe wakijipima nafsi zao na nafsi zao, na wakijilinganisha nafsi zao kwa nafsi zao, hawana akili.*"

Paulo alisema kuthibitishwa na wengine ni jambo dogo. 1 Kor. 4:3, "*Lakini kwangu mimi si kitu kabisa nihukumiwe na ninyi, wala kwa hukumu ya kibinadamu, wala sijihukumu hata nafsi yangu.*"

Mara nyingi watu hukosea katika mawazo yao na kuchanganua mambo. Wengi watajikuta wamepotea Siku ya Hukumu. Mat. 7:13-14, "*Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache.*"

Bado tunapaswa kuangalia kiwango kingine ambacho tunapaswa kujichunguza wenyewe.

Tunapaswa kujijaribu wenyewe kwa kiwango cha neno la Mungu.

Tena, ni pendekezo la Bwana ndilo linalomfanya mtu ajithibitishe. 2 Kor. 10:18, "*Maana mtu mwenye kukubaliwa si yeye ajisifuye, bali yeye asifiwaye na Bwana.*"

Ni Bwana ndiye hakimu aliye halali. 1 Kor. 4:4, "*Maana sijui sababu ya kujishitaki nafsi yangu, lakini sihesabiwi haki kwa ajili hiyo; ila anihukumuye mimi ni Bwana.*"

Kama Bwana mwenyewe alivyosema, tutahukumiwa kwa maneno yake. Yoh. 12:48, "*Yeye anikataaye mimi asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho.*"

Kiwango pekee kizuri cha kutumia tunapojichunguza wenyewe ni Neno la Mungu. Hatuwezi kuamini hisia zetu, au kile ambacho wengine wanasema.

Mwisho, hebu nilete baadhi ya...

Maswali yanayoweza kutusaidia kujichunguza wenyewe

Je Kristo yu ndani yangu?

Je nimemvaa katika ubatizo? Gal. 3:27, "*Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*"

Je nazishika amri zake?

Yoh. 14:21, "*Yeye aliye na amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu, nami nitampenda na kujithihirisha kwake.*"

Je "alama" za utume ziko katika maisha yangu?

Je ninakaa katika neno lake? Yoh. 8:31, "*Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli.*"

Je ninawapenda ndugu zangu kama Kristo alivyonipenda?

Yoh. 13:34-35, "*Amri mpya nawapa mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.*"

Je ninazaa matunda?

Yoh. 15:8, "*Hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi wangu.*"

- Matunda kama ya Rohoni. Gal. 5:22-23, "*Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi, juu ya mambo kama hayo hakuna sheria.*"
- Matunda kama ya kazi njema. Tit. 2:14, "*Ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema.*"

Je nina nia kama ya wale waliokuwa wanafunzi wa kweli?

Akiwa katika uvuvio, Paulo anaandika 2 Kor. 13:6, picha ya akili yake ilikuwaje? 2 Kor. 13:6, "*Lakini natumaini kama mtajua ya kuwa sisi hatukukataliwa.*"

Tunaweza kuwa na akili kama ya mwanafunzi wa kweli(Paulo) kutoka katika barua yake kwa Wafilipi: Fil. 3:7-14, "*Lakini mambo yale yaliyokuwa faida kwangu, naliyahesabu kuwa hasara kwa ajili ya Kristo. Naam, zaidi ya hayo nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu; ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo; tena nionekane katika yeye, nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani; ili nimjue yeye na*

uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake; ili nipate kwa njia yo yote kuifikia kiyama ya wafu. Si kwamba nimekwisha kufika, au nimekwisha kuwa mkamilifu; la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu. Ndugu sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo niifikie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu."

- Sasa, tunasoma malengo yake katika maisha (7-11)
- Tunasoma kuhusu nia yake katika kupata lengo hilo (12-14). Rudia kusoma kifungu hiki na ujifunze maana ni mifano mizuri ya kuishi kwalo.

WOTE tutakuwa na "*picha hii*" kama tukiwa "*katika imani*" na "*Kristo yu ndani yetu*". Fil. 3:15-17, "*Basi sisi tulio wakamilifu na tuwaze hayo; na hata mkiwaza mengine katika jambo lo lote, Mungu atawafunulia hilo nalo. Lakini hapo tulipofika na tuenende katika lilo hilo. Ndugu zangu mnifuate mimi, mkawatazame wao waendao kwa kuufuata mfano tuliowapa ninyi.*"

Hebu na sisi sote tuwe na nia kama hiyo kwamba Paulo alikuwa anajali mienendo yetu, tukijichunguza wenyewe kwamba tuko katika njia sahihi.

Hitimisho

Maswali mengine yaweza kuwa vyema kujiuliza unapojichunguza mwenyewe, lakini natumai kwamba maelezo haya jinsi ya kutumia Neno la Mungu katika "*kujithibitisha*" sisi wenyewe.

Zingatia huzuni mbaya ya hao "*wanaoachwa*", "hawaja hitimu", walio "shindwa jaribio".

Kuhakikisha kwamba "*hautashindwa*", basi kila mara "*jichunguze mwenyewe*" katika mwanga wa Neno la Mungu!